*Check Against Delivery*

# HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA BENJAMIN WILLIAM MKAPA, KWA WANANCHI, 30 SEPTEMBA 2003

Ndugu Wananchi,

Mtakuwa mmesikia kuwa tarehe 8 na 9 mapema mwezi huu niliwakusanya Mawaziri wote, Naibu Mawaziri wote, Makatibu Wakuu wote, Naibu Makatibu Wakuu wote, baadhi ya viongozi wa taasisi za fedha, wawakilishi wa makundi mbalimbali katika jamii, kama vile wafanyakazi, wafanyabiashara, Asasi Zisizokuwa za Serikali, na wengine wengi, kujadili jambo moja tu: Namna ya kusaidia sekta isiyo rasmi iondokane na unyonge wa kutengwa na mfumo rasmi wa sheria na uchumi nchini; na namna ya kusaidia raslimali nyingi iliyo katika sekta hiyo igeuke kutoka raslimali iliyokufa na kuwa raslimali hai, inayoweza kuwa chanzo cha mitaji ya kupanua shughuli za uchumi kwa kujitegemea sisi wenyewe.

Tulimwalika mtaalamu anayetambulika duniani kama kinara wa mageuzi ya aina hiyo, Bw. Hernando de Soto, raia wa nchi ya Peru, aje atuelezee uzoefu wake wa kubuni suluhisho la matatizo ya aina hii yanayoikabili sekta isiyo rasmi kwenye nchi zote zinazoendelea. Kazi hiyo ameifanya kwa miaka mingi nchini kwao Peru, kwenye nchi za Ulaya Mashariki, nchi za bara la Asia na barani Afrika, nchini Misri. Tanzania ni nchi pekee Kusini mwa Jangwa la Sahara ambayo Bw. de Soto anashughulika nayo.

Kuna sababu mbili kubwa zilizonifanya nichukue hatua hii.

Kwanza, nina wajibu wa kuongoza vita dhidi ya umaskini, kwa mwongozo uliopo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM, na Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka 2000 – 2010, mwongozo unaoweka mkazo kwenye **uwezeshaji wa wananchi kujiendeleza**.

Kijitabu cha Mwelekeo wa Sera kina sura nzima, Sura ya Tatu, kuhusu "Mikakati ya Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Wananchi". Sehemu ya Ibara ya 51 iliyopo kwenye sura hiyo inasema:

> "Mkakati wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ni njia inayobuniwa kuwafanya Watanzania walio wengi nao waweze kumiliki na kuendesha

uchumi katika nchi yao. Dhana kuu hapa ni **uwezeshaji**, yaani kuunda mazingira muafaka yatakayowapatia fursa za kumiliki ardhi, viwanda na zana za kazi, kupata mitaji ya kuwekeza katika shughuli za kiuchumi, kupata elimu na maarifa ya kuendesha biashara na miradi ya kiuchumi, n.k. Katika utekelezaji wa mikakati ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, vijana na wanawake wapewe kipaumbele."

Kwa upande wake, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2000 ilisema ifuatavyo kwenye Ibara ya 6:

"Chama cha Mapinduzi kimebuni mkakati wa **uwezeshaji wa wananchi kiuchumi** ambao utawafanya Watanzania walio wengi nao waweze kumiliki na kuendesha uchumi katika nchi yao. Dhana ya **uwezeshaji** maana yake ni kuunda mazingira mwafaka yatakayowapatia Watanzania fursa ya kumiliki na kuendesha uchumi wa nchi yao."

Ndugu Wananchi,

Wananchi wetu wengi sana wanafanya shughuli zao zote, au sehemu ya shughuli zao, kwenye sekta isiyo rasmi. Wana raslimali, lakini raslimali zenyewe hazitambuliwi kisheria na hivyo haziwezi kuwapa fursa ya kupata mitaji ya kupanua shughuli zao kwa kukopa. Wakati huo huo benki nyingi nchini zinashikilia fedha nyingi ambazo zingeweza kutumika kuwakopesha mitaji. Kwa wananchi wengi hawa uwezeshaji wa kweli si wa kuwapa mikopo midogo midogo tu, bali pia uwezo wa kupata mikopo mikubwa zaidi baada ya raslimali zao kutambulika kisheria. Mikopo midogo, inayoweza kutolewa bila watu kuweka raslimali zao rehani, inaweza kusaidia kuanzisha na kuendeleza miradi midogo ya kuwapa wananchi fedha za kula. Ni jambo muhimu, na tutaendelea nalo. Lakini tukiridhika nayo watu wetu watabaki wadogo kwenye uchumi daima. Mimi nataka Watanzania wengi zaidi watoke kwenye uchumi wa kujikimu, waende kwenye uchumi mkubwa wa kuzalisha ziada. Hapo ndipo Watanzania kweli watamiliki uchumi wa nchi yao. Kudai wananchi wamiliki uchumi bila kwanza kuwawezesha kufungua kufuli zilizofungia raslimali zao ni kujidanganya. Tuwasaidie wananchi kuachana na udogo wa uchumi wao, maana hii ni nchi yao. Lakini hiyo ni kazi kubwa sana, inayohitaji mabadiliko

makubwa ya fikra na mtazamo, na wala hakuna njia ya mkato kama wengine wanavyofikiri.

Sababu ya pili iliyonisukuma kuchukua hatua hii ni mafanikio tuliyoyapata, na tunayosifiwa nayo, ya kuboresha uchumi mkuu. Tumesifiwa sana kote duniani kwa kazi kubwa tuliyoifanya, na mafanikio ya mageuzi yetu ya uchumi, na utulivu kisiasa. Lakini kama wengine wanavyopenda kusema, na sisi Serikali tunavyokiri, mageuzi ya uchumi, na kuboresha uchumi mkuu, peke yake haitoshi kupambana na umaskini. Maana umaskini ni kama pweza, ana mikia mingi. Mageuzi ya uchumi na ubora wa uchumi mkuu ni hatua muhimu sana ya kwanza katika safari ndefu ya kuepukana na umaskini, lakini kamwe si mwisho wa safari.

Hivyo, nimeona wakati sasa umefika wa kuchukua hatua inayofuata, nayo ni kuhakikisha manufaa ya uchumi mkuu ulio bora, na uliotulia, yanawafikia wananchi wengi zaidi. Na hatua hii ndiyo hasa inahitaji uwezeshaji wa wananchi kwa elimu, kwa ujuzi, na kwa mitaji. Mradi huu tunaotarajia kuuanza unalenga uwezeshaji kwa mitaji, na unalenga kutambua na kutafuta suluhisho la matatizo yanayowakabili walio katika sekta isiyo rasmi watakapo kupanuka au kuingia kwenye mfumo rasmi wa kisheria na kibiashara nchini.

Mradi huu si kitu cha ajabu, kilicho nje ya mikakati mingine ya kupiga vita umaskini na uwezeshaji wananchi ambayo tumeianza na ambayo tutaendelea nayo. Huu si mradi mbadala, ni nyongeza tu. Mradi huu unalenga kutafuta suluhisho la tatizo la kipekee la raslimali za watu wetu kutotambulika kisheria, na kwa hiyo kuwa raslimali zilizokufa kisheria. Ni utajiri uliofungwa kwenye raslimali zilizokufa. Changamoto ni kufufua raslimali hizo, na kwa kufanya hivyo, kufungua milango ya mitaji mikubwa kwa wananchi kujiendeleza na kutajirika, si kuishi kwa kujikimu tu. Tunataka tuwawezeshe wananchi watajirike kihalali, ndani ya mfumo rasmi, wa kisasa, na wa kisheria.

**<u>Mradi ni Wetu</u>**

Wapo wanaoweza kuwa na mashaka iwapo matatizo yetu kama haya ya maendeleo yanaweza kutatuliwa na wataalam kutoka nchi za nje. Napenda kuwahakikishieni, Ndugu Wananchi, kuwa mradi wa kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayoikabili sekta isiyo rasmi ni wetu, wala si wa wageni. Kinachotekelezwa ni sera za CCM, kama nilivyozinukuu, na wala si sera za mtu mwingine yeyote nje au ndani ya nchi.

Utaalamu tunaouhitaji na kuukaribisha ni ule wa kutusaidia kufanya kile ambacho wenyewe tulishaamua kukifanya. Ni sawa na kwenda dukani kununua jembe. Jembe halina shamba, wala halimtumi mkulima kufanya asichokitaka. Jembe linamsaidia tu mkulima kulima pale alipoamua mwenyewe kulima. Na utaalam tunaouagiza kutoka nje ni chombo tu cha kutusaidia kutimiza malengo yetu wenyewe.

Na kwa kweli wataalam kutoka nje watakuwa wachache sana. Kazi kubwa itafanywa na Watanzania wenyewe, wanaoelewa mazingira na hali halisi ya nchi yetu. Tunachopata kutoka nje ni mifupa tu, nyama na mishipa itatokana na sisi wenyewe.

Tunahitaji pia kiasi kikubwa cha msaada wa fedha kugharamia kazi hii. Kwa niaba yenu naishukuru Serikali ya Ufalme wa Norway ambayo imegharamia semina yetu, na sehemu hii ya kwanza. Matarajio yangu ni kuwa tutaelewana nao namna ya kuendelea kushirikiana katika hatua zinazofuata.

**Utafiti**

Ndugu Wananchi,

Hatua itakayofuata ni kutafiti hali halisi ya sekta isiyo rasmi. Mipango yoyote ya maendeleo inahitaji takwimu, inahitaji kujua hali halisi. Hatuwezi kuwasaidia walio katika sekta isiyo rasmi kutumia raslimali zao kupata mitaji iwapo hatujui wana nini. Hatuwezi kubuni sheria, kanuni na taratibu zitakazowarahisishia kuingia kwenye sekta rasmi iwapo hatujui mifumo na mitandao ya ufanyaji kazi, biashara na mikataba ya kienyeji itumikayo kwenye sekta isiyo rasmi. Hatuwezi kwenda mbele na mradi huu kama hatujui vikwazo wanavyokabiliana navyo walio katika sekta isiyo rasmi wakitaka kutambuliwa kisheria. Tumefanya huko nyuma sensa au uchunguzi wa thamani na hivyo utajiri wa kaya moja moja *(Budget Household Survey)*. Vigezo tulivyotumia kupima viliamuliwa na nani na kwa ushiriki wetu wa kiasi gani? Kuna uwezekano mkubwa kwamba vigezo hivi na sensa hizi ni vya mali au mapato bubu, au mfu!!

Kwa hiyo, tutakuwa na kazi kubwa ya kutafiti na kuchambua kujua nani anamiliki nini, wapi, na haki zake. Hiyo ni hatua ya kwanza iwapo hatimaye tutaweza kumpa kila mwenye raslimali haki ya kutambuliwa na sheria za nchi kuwa mali ile kweli ni yake, na anaweza kuitumia apendavyo, ikiwemo kuitumia kama rehani kupata mikopo ya mitaji ya kuendeleza biashara na shughuli zake.

Kwa wale wanaosafiri kwa ndege wanajua kuwa ukifika uwanja wa ndege unakabidhi sanduku lako, lenye mali zako zote unazosafiri nazo. Na unapewa

kipande kidogo tu cha karatasi, ambacho chenyewe hakina thamani yoyote. Lakini utakitunza sana, maana mwisho wa safari hicho ndicho utawakabidhi wenye ndege kama ushahidi kuwa sanduku unalotaka kulichukua mwisho wa safari ni lako. Hali kadhalika katika uchumi wa soko, uchumi uliotanda dunia ya leo. Bila karatasi inayotambulika kitaifa au kimataifa, inayoonyesha wazi kuwa nyumba fulani, shamba fulani, mifugo fulani, mazao fulani, kiwanda kidogo fulani, au hata cherehani fulani, ni mali yako, na vina thamani ya kisheria, huwezi kuvitumia vitu hivi kama rehani ya kukopa mitaji. Na uchumi wa kisasa unaendeshwa hivyo—kwa mikataba, kwa kukopa, kwa kuweka rehani, na kwa uaminifu wa kulipa.

Lakini haitoshi kwa Serikali kujua nani anafanya nini, au ana nini, kwenye sekta isiyo rasmi. La muhimu pia ni kujua hawa watu wengi walio katika sekta isiyo rasmi wanakwamishwa na nini hata washindwe kutambuliwa kisheria na kuingia kwenye mkondo rasmi wa uchumi wa taifa.

Hivyo utafiti utakaofanywa utatusaidia kujua vikwazo hivyo, ikiwamo vikwazo vya kisheria, taratibu, na kanuni za Serikali Kuu, au Serikali za Mitaa. Utafiti ambao Bw. de Soto ameufanya nchini Misri, kwa mfano, umeonyesha kuwa mtu akitaka kufungua biashara rasmi ya kuoka mikate, itamchukua siku 540, akitoka ofisi moja kwenda nyingine, na gharama yake kupata hiyo leseni ni mara 84 ya wastani wa mshahara wa mtu kama yeye. Na hiyo ni nchi yenye uchumi mkubwa zaidi kuliko sisi. Sijui utafiti wetu sisi utaonyesha nini.

Kwa sasa, ninachotaka kusema ni kuwa japo huko nyuma tumejitahidi sana kuielewa sekta isiyo rasmi, lakini tulikuwa hatujafanya utafiti mpana kama huu tunaoukusudia, ambao si tu utaonyesha raslimali nyingi isiyo katika sekta rasmi, bali itatusaidia kutambua ukubwa wa utajiri ulio nje ya sekta rasmi. Safari hii tutataka pia kujua undani wa shughuli zifanywazo nje ya sekta rasmi ili zitambulike, na wenye raslimali watambulike kisheria, na vikwazo vinavyowazuia kuingia kwenye sekta rasmi, itakayofungua milango kwa mali hizo kugeuka mitaji, vijulikane ili tuanze kazi ya kuviondoa kimoja baada ya kingine.

**Tafiti nyingi zilizopita ziliangalia sekta isiyo rasmi kama tatizo. Tafiti zijazo lazima zilenge katika kuinua sekta isiyo rasmi kama chanzo cha utajiri na mitaji, na kuangalia Serikali kama mojawapo ya matatizo. Lazima sisi katika Serikali tubadilike, tukubali kuchunguzwa, ili kama sheria zetu, taratibu zetu, na kanuni zetu ni tatizo, kama ni kizingiti mlangoni kinachozuia walio nje ya sekta rasmi wasiingie, basi tuvishughulikie vizingiti hivyo.**

Mimi nina uhakika kuwa, kama ilivyotokea nchini Misri, hapa pia tutashituka sana tutakapojua kiwango halisi cha utajiri wa nchi hii kilichopo nje ya sekta rasmi. Kule Misri watafiti hawa waligundua kuwa watu 9 kwa kila 10 walikuwa na raslimali, na kufanya aina fulani ya biashara, nje ya mfumo rasmi. Raslimali hizo, zilizo katika sekta isiyo rasmi, zilikuwa na thamani ya sh.245 trilioni (USD 245 bn), kiasi ambacho ni mara 55 ya mitaji kutoka nje ya Misri iliyowekezwa ndani ya nchi hiyo; au mara 30 ya thamani ya biashara ifanywayo ndani ya sekta rasmi.

Utafiti huo uligundua pia kuwa utajiri huo mwingi ulibaki nje ya mfumo rasmi kwa sababu ya gharama na vikwazo lukuki kwa anayetaka kuingia kwenye sekta rasmi. Kwa mfano, ilichukua miaka 2 kupata leseni ya biashara, na miaka 17 kupata hati ya nyumba ili iweze kutumiwa kukopa benki.

## Ufumbuzi

Ndugu Wananchi,

Kazi tunayotaka kuianza ni kubwa, ya gharama kubwa, itakayochukua muda mrefu. Haina lengo la kuwabughudhi wananchi walio katika sekta isiyo rasmi, wala siyo mkakati wa kukusanya kodi. Na wala huu si mwarobaini wa kumaliza matatizo yetu yote. Lakini, utashi wa kisiasa wa viongozi wetu kutambua kuwa hatuwezi kushinda vita dhidi ya umaskini iwapo hatutawasaidia wananchi wenye raslimali zao, na biashara zao, nje ya mfumo rasmi nao wanaingia kwenye mfumo rasmi. Tunawaita maskini, lakini kiasi fulani cha umaskini wao kinachangiwa na kukosa fursa za kugeuza raslimali zao kuwa mitaji ya kupanua shughuli zao, na kutimiza ndoto zao, na mahitaji yao.

Tunahitaji utashi mkubwa wa kisiasa kuacha kuwaona walio katika sekta isiyo rasmi kuwa ni tatizo, bali ya kuwaona kama ufumbuzi wa matatizo ya umaskini na udogo wa mitaji na masoko ya bidhaa. Tunahitaji utashi wa kisiasa kukubali kujichunguza Serikali iwapo kweli sisi ni sehemu ya tatizo, au la. Na kama jibu ni ndio tuwe tayari kubadilika haraka.

Katika kipindi kilichobaki cha Urais wangu nitaweka mkazo mkubwa sana katika kusukuma kujengeka kwa utashi huo wa kisiasa. Najua si kazi rahisi. Maana wapo wanaofaidi na mfumo uliopo ambapo shughuli nyingi za wananchi zinakuwa nje ya mfumo rasmi wa sheria za nchi. Wapo wanaoshiba kwa kudai rushwa ili wasibomoe nyumba au vibanda vilivyopo nje ya mfumo rasmi. Wapo wanaoshiba kwa kuwazungusha wanaotafuta leseni ili wafanye biashara ndani ya mfumo wa

sheria. Wapo wanaoshiba kwa kila kibali ambacho mwananchi anahitaji ili kuingia katika sekta rasmi. Na pengine juu yao wapo wakubwa wachache wanaopata sehemu ya mapato ya udhalimu huo.

Watu wa aina hiyo ndio watapinga au kujaribu kuhujumu mabadiliko tunayotaka kuyaleta. Lakini hoja haipingiki. Lazima tufungue milango ndugu zetu walio nje waingie ndani ya mfumo rasmi wa kisheria, kiutawala na kibiashara. Tumesubiri kwa miaka mingi ije misaada na mitaji kutoka nje ya kutosha kuleta mageuzi ya haraka katika maisha yetu na maendeleo ya taifa. Baada ya miaka 42 ya Uhuru sasa tumetambua kuwa kasi hiyo ya misaada na mitaji kutoka nje itatufanya tubaki maskini kwa miaka mingi. Lakini tumejua pia kuwa katika miaka hiyo 42 zipo raslimali nyingi zilizopatikana, zilizopo mikononi mwa wananchi wetu, lakini ni kama vile Serikali imezifumbia macho, haizioni, ingawa nadhani ni kubwa kwa viwango ambavyo havitapishana sana na hali iliyogundulika kule Misri. Kama hivyo ndivyo, ufumbuzi wa haraka, na wa kwanza, lazima uwe kufunguliwa raslimali zilizo nje ya mfumo rasmi, ili zijenge uwezo mpya wa wananchi kupanua shughuli zao, kuboresha maisha yao bila hofu, au kudaiwa rushwa watafutapo riziki zao.

Najua wapo wenye mashaka, ndani na nje ya Serikali. Mageuzi makubwa duniani yanaletwa na walio jasiri; wanaothubutu. Naomba Watanzania tuwe watu wa aina hiyo.

Mungu Ibariki Afrika!
Mungu Ibariki Tanzania!

Asanteni kwa kunisikiliza.